

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE

SHULE YA SEKONDARI DINDIRA,
S.L.P 675,
KOROGWE.

KUMB Na. DSS/FI/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DINDIRA WILAYA YA KOROGWE MKOANI TANGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Nakupongeza kwa kuchaguliwa kuendelea na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza mwaka 2021 na kupangwa katika shule ya Sekondari Dindira. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na uwe umefika shuleni muda wa saa 1:00 asubuhi ukiwa na mzazi/mlezi wako. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU KUZINGATIA

2.1 Sare ya shule kwa wanafunzi wa kiume(wavulana)

- i. Suruali mbili kitambaa kizito rangi damu ya mzee isiwe inabana. Kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu hii.
- ii. Mashati mawili ya mikono mifupi tetron/tomato rangi nyeupe.
- iii. Viatu jozi mbili vya kufungwa kwa kamba rangi nyeusi.
- iv. Sweta 1 damu ya mzee.
- v. Soksi jozi 2 rangi nyeusi.
- vi. Mkanda wa ngozi mweusi.
- vii. Tai rangi ya damu ya mzee.

1.1 Sare ya shule kwa wanafunzi wa kike (wasichana)

- i. Sketi 2 kitambaa kizito rangi ya damu ya mzee - rinda box.
- ii. Mashati 2 ya mikono mifupi tetron/tomato rangi nyeupe.
- iii. Viatu jozi 2 vya kufungwa kwa kamba rangi nyeusi.
- iv. Sweta 1 rangi ya damu ya mzee.
- v. Soksi jozi 2 rangi nyeupe
- vi. Hijabu inaruhusiwa ila ifanane na sare ya shule (kwa muislam)

1.2 vifaa vya kujifunzia

- i. Counter Book quire 2 au 3 yawe 10.
- ii. Kalamu 2 na penseli 2.
- iii. Mkebe wenye vifaa vyote. (Mathematic instruments)

2.4 Vifaa vya usafi na utunzaji wa mazingira.

- i. Ndoo 1 ndogo ya ujazo wa lita 10 plastiki.
- ii. Fagio 1 aina ya ukindu/chelewa.

3.0 KANUNI ZA SHULE

- i. Kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote
- ii. Kutekeleza taratibu za shule kwa mtiririko wake kama inavyo oneshwa
- iii. Kuwa na maadili mema wakati wote

4.0 SHERIA ZA SHULE

Zinakataza kufanya au kuwa na tabia zifuatazo;

- i. Wizi
 - ii. Ubakaji.
 - iii. Uasherati na ushoga.
 - iv. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.
 - v. Kupigana na kupiga.
 - vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
 - vii. Kudharau bendera ya taifa.
 - viii. Kupata mimba nakuendelea kuishi na ujauzito ukiwa shule.
 - ix. Kuoa na kuolewa.
 - x. Kutoa mimba
 - xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
 - xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
 - xiii. Kuwa na simu ya mkononi.
- NB; Makosa haya yata kufukuzisha shule.

5.0 FOMU YAKUONYESHA AFYA YAKO KABLA YA KUJIUNGA NA SHULE (MEDICAL EXAMINATION FORM)

➤ Fomu hii inajitegemea na inapaswa kujazwa kikamilifu.

Ni matumaini ya jumuiya ya shule hii na viongozi wa shule kuwa utatekeleza maagizo namba 1 hadi 5 hapo juu kwa weledi wa hali ya juu.

KARIBU SANA.

SHEMADANGA R.D.

MKUU WA SHULE

0654896979